Jarida la Wizara ya Afya

# Afya Habari

JARIDA LA MTANDAONI LA WIZARA YA AFYA | TOLEO, NO. 9, JULAI 2023



# TUNABORESHA AFYA

MTU NI AFYA, JALI AFYA YAKO

# TAHARIRI

Kwa niaba ya Uongozi, Menejimenti na Watumishi wote wa Wizara ya Afya napenda kukukaribisha ndugu msomaji wa jarida hili lililosheheni habari za matukio muhimu ya Wizara ya Afya na Sekta ya Afya kwa ujumla wake.

Kwa kudra zake Mwenyezi Mungu tumevuka Mwezi wa Saba na tumeanza tayari mwaka mpya wa Bajeti ya Serikali mwaka 2023/24. Bunge la Jamhuri la Muungano wa Tanzania mnamo Mei 15, 2023 lilipitisha na kuidhinisha Bajeti ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya ya Shilingi Trilioni 1.2.

Tunaamini chini ya uongozi wa Rais wetu mpendwa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Viongozi wetu wa Wizara wakiongozwa na Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu na msaidizi wake Mhe. Dkt. Godwin Mollel Naibu Waziri wa Afya, tunakwenda kuboresha zaidi utendaji kazi wa watumishi wetu kuhakikisha kuwa miundombinu iliyojengwa, wataalam walioletwa na Serikali, Dawa na Vifaa tiba vinavyonunuliwa na Serikali vinaenda kutoa thamani halisi ya ya ubora wa huduma za matibabu kwa wananchi wetu.



Sisi tukiwa watendaji ndani ya Wizara tutaendelea kuhakikisha tunakuwa wabunifu, kufanya kazi kwa juhudi ili kuhakikisha azma ya Serikali yetu pendwa inatekelezwa kikamilifu kwa kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za afya.

**Dkt. Seif Shekalaghe**
**KATIBU MKUU WIZARA YA AFYA**

Skani kwa kutumia kamera
ya Simu yako kupakua kidigitali
Jarida hili.




## BODI YA UHARIRI

**MWENYEKITI**
Dkt. Seif Shekalaghe
KATIBU MKUU

**MHARIRI**
Englibert Kayombo

**WAHARIRI WASAIDIZI**
Catherine Sungura
Emmanuel Malegi

**WAJUMBE**
Englibert Kayombo
Catherine Sungura
Emmanuel Malegi
Rayson Mwaisemba
Majid Abdulkarim
Said Nyaoza
Hassan Kimweri
Peter Mabwe

**WASANIFU**
Englibert Kayombo
Said Nyaoza

@wizara_Afyatz
www.moh.go.tz

# YALIYOMO

Muhimbili nyingine kujengwa Kigoma.... UK 2





Ubora wa Huduma wamkosha Waziri Mkuu.... UK 3

Waziri Mkuu aweka jiwe la msingi jengo la Wagonjwa wa nje Hospitali ya Ligula - Mtwara .... UK 4





Wakina Mama 98 wapona Saratani ya Shingo ya Mlango wa Kizazi Tanzania..... UK 5

Kanada yatoa Shilingi Bilioni 140 kwenye Mfuko wa Afya wa Pamoja.... UK 6





Serikali kupunguza Uagizaji wa Bidhaa za Afya Kutoka 80% Hadi 50% Ifikapo 2030.... UK 7

Serikali kushirikiana na TAMWA katika masuala ya Afya ya Uzazi Mama na Mtoto.... UK 8



Watu 86 Mkoani Tanga kufanyiwa Upasuaji wa Kurekebisha Viungo.... UK 10





Wizara ya Afya yakabidhi Zimamoto Magari ya Uokoaji yenye Thamani ya Bilioni 1.6 .... UK 11

Kigoma kupata Ambulance 17 kwaajili ya kubebea Wagonjwa .... UK 18





"Shirika la Madaktari Afrika" lasaidia JKCI Vifaa Tiba vya Bilioni Moja... UK 16

Dkt.. Mollel aahidi Mashine ya CT Scan Hospitali ya Ligula - Mtwara .... UK 17





Watoa huduma za Afya Nchini watakiwa kutoa huduma bora kwa matarajio ya Wananchi .... UK 19

Wamiliki wa Maduka ya Dawa Nchini fuateni utaratibu sahihi wa utoaji wa Dawa .... 20





Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa Kinara katika kuboresha Huduma za Utengamao na Tiba Mazoezi, Matengenezo ya Vifaa Tiba na Miundombinu.... UK 21



Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya kujikita katika Ubingwa Bobezi na Tiba Utalii .... UK 22

Dkt. Kikwete akoshwa na Huduma za Muhimbili .... UK 24





Chalamila awataka Wananchi kuzingatia ushauri wa Wataalamu wa Afya kuepuka Magonjwa. .... UK 25

wizara ya afya yazindua utafiti wa kitaifa wa viashiria vya magonjwa yasiyoambukiza .... UK 26





Mashine ya MRI imeanza kufanya kazi Hospitali ya Rufaa ya Kanda - Mbeya .... UK 27

MUHIMBILI imekidhi vigezo kushughulikia dharura za AFCON 2027 ... UK 28





Upasuaji wa Miguu kifundo kufanyika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita .... UK 30

# Rais Samia atoa Milioni 2 kwa Mariam anaesaidia Watoto Njiti kwa kuwapa joto





Na Englibert Kayombo

Rais wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ametuma salamu za pongezi kwa Mariam Mwakabungu (25) anayejitolea kukumbatia watoto njiti waliotelekezwa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Amana jijini Dar es Salaam.

Ujumbe huu ulitumwa siku moja tangu mitandao ya Mwananchi Julai 18, 2023 iliporipoti habari kuhusu Mariam na namna alivyosaidia watoto watatu waliotelekezwa na mama zao.

Rais Samia alituma ujumbe huo leo Jumatano, Julai 19, 2023 uliwasilishwa na Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk Brayson Kiwelu ambaye amemkabidhi Mariam kiasi cha Sh2 milioni.

Dk Kiwelu alisema ujumbe huo umetumwa na Rais Samia ambaye amekuwa mstari wa mbele katika huduma za mama na mtoto.

"Rais ametoa Sh2 milioni fedha taslim kumpatia mama huyu kwa kujitoa kwake na amewapongeza viongozi wa Wizara ya Afya na Amana kwa ubunifu huu na uthubutu mama huyu kuwa sehemu yetu", alisema.

"Rais ameshukuru sana msaada ambao mama huyu ameutoa na amewataka Watanzania kuendelea kujitoa kwa ajili ya kuhudumia wale wenye uhitaji," alisema Dk Kiwelu.






# Muhimbili nyingine kujengwa Kigoma

**Na Rayson Mwaisemba**
**Kigoma**

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Philip Isdor Mpango amesema Serikali imedhamiria kujenga hospitali ya Rufaa ya kanda ya Magharibi yenye hadhi sawa na hospitali ya Taifa Muhimbili itayosaidia kuondoa changamoto ya Rufaa za wagonjwa walioku-wa wakitibiwa katika hospitali za Rufaa za Mbeya, Benjamin Mkapa na Muhimbili.

Dkt. Mpango alisema hayo wakati akizindua hoteli ya Bwami Dubai iliyopo Kasulu Mkoani Kigoma, ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake ya kuzindua miradi mbalimbali Mkoani Kigoma.

"Pale Kigoma tunajenga hospitali ya kanda, lakini sio hivyo tu vyuo vikuu mnasikiaga vipo Dar es Salaam, kwahiyo chuo kikuu cha tiba Muhimbili wamekuja kuanzisha tawi la chuo kikuu Kigoma na kitakuwa sambamba na hiyo hospitali ya kanda." alisema.

Aliendelea kusema, pamoja na kujengwa kwa Zahanati ya Kasumo bado Serikali iliona haja ya kuwa na hospitali hiyo ya kanda ili wananchi wa Mkoa wa Kigoma pamoja na nchi za jirani waweze kunufaika na huduma hizo jambo litalosaidia kupunguza Rufaa katika Mikoa ya Dodoma.

Aidha, Mhe. Dkt. Mpango alitoa wito kwa wananchi wa Mkoa huo kuwalisha watoto lishe inayofaa kwa afya ili kuwaongezea uwezo wa akili, huku akiwataka Wataalamu wa masuala ya lishe kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa kuwapa lishe bora watoto ili kuinua kiwango cha elimu kwa watoto wao.

Naye Naibu Waziri wa Afya Dkt. Godwin Mollel alisema, katika Sekta ya Afya kuanzia ngazi ya Hospitali ya Mkoa mpaka zahanati Mkoa umepokea kiasi cha Shilingi Bilioni 49 iliyosaidia kununua vifaa tiba vya kisasa, kuboresha miundombinu ya kutolea huduma ili wananchi wa Kigoma wapate huduma bora.

Alisema, kwa uwekezaji mkubwa wa Trilioni 1.3 uliopewa na Serikali ya Rais Samia katika Sekta ya Afya umesaidia kupunguza Rufaa za wagonjwa kwenda kutibiwa nje ya nchi, na kusisitiza uwekezaji huo umesaidia kuongeza idadi ya wagonjwa kutoka nje ya nchi wanaokuja kutibiwa ndani ya Tanzania (medical tourism).

Aliongeza, kuwa tayari Mkoa wa Kigoma umeanza kutoa huduma za CT-SCAN kwa wananchi wa Mkoa wa huo na nchi jirani, huduma ambazo zilikuwa zikitolewa katika Mikoa ya Mbeya na Dodoma, na kuweka wazi zaidi ya watu 464 tayari wamepatiwa huduma za vipimo na mashine hiyo ya CT-SCAN tangu ilipoanza kutoa huduma hiyo mapema mwezi Januari mwaka huu.



# Ubora wa Huduma wamkosha Waziri Mkuu

**Na. Mwandishi Wetu,**
**Dar ES Salaam**

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa ameipongeza Wizara ya Afya kupitia Hospitali ya Taifa Muhimbili kwa kuboresha huduma na mazingira ya Hospitali hiyo.

Mhe.Majaliwa alisema hayo  Julai 23, 2023 alipotembelea Hospitali hiyo kumjulia hali mgonjwa aliyelazwa hapo ambaye anaendelea vizuri na kupata fursa ya kuwasalimia wagonjwa wengine.

"Nimefurahishwa sana jinsi mlivyoboresha huduma, wakati napita kusalimia baadhi ya wagonjwa wamenieleza kuridhishwa na huduma wanazopatiwa, hii inatia moyo sana", alisema Mhe. Majaliwa.

"Nimefurahishwa nauboreshaji wa mwonekano wa Hospitali, mazingira, majengo na hii ndio Hospitali ya Taifa Muhimbili tunayoitaka" alisema Mhe.Majaliwa.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, Prof. Mohamed Janabi alimhakikishia Mhe. Majaliwa kuwa Menejimenti itaendelea kuimarisha huduma zake katika nyanja mbalimbali.












# Waziri Mkuu aweka jiwe la msingi jengo la Wagonjwa wa nje Hospitali ya Ligula - Mtwara

**Na. Emmanuel Malegi,
Mtwara**

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa ameweka jiwe la msingi katika jengo jipya la wagonjwa wa njee (OPD) katika hospitali ya rufaa ya Mkoa wa Mtwara-Ligula, jengo hilo ni la mradi ambao ni wa zaidi ya Bilioni 4 ambao unasimamiwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC).

Aidha waziri Majaliwa aliagiza mkandarasi wa ujenzi huo shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kuendelea na ujenzi huo kwa awamu ya pili ili jengo hilo liweze Kukamilika na kutumiwa na wanachi ili kurahisisha uboreshwaji wa huduma za afya kwa wakazi wa Mtwara na kusini kwa ujumla.

Akizungumza mara baanda ya kuweka jiwe la msingi Mhe.Majaliwa alielekeza watumishi wafanye kazi kwa kujituma, weredi na uaminifu.

Pia Mhe Majaliwa alisisitiza kuwa mradi huo ni moja ya miradi mingi ya mabilioni inayotekelezwa katika jimbo la mtwara fedha zinazotolewa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kupitia Wizara ya Afya.






# Wakina Mama 98 wapona Saratani ya Shingo ya Mlango wa Kizazi Tanzania

**Na Said Nyaoza,**
**Dodoma**

Serikali imesema NBC Marathon Dodoma ndani ya miaka mitatu imefanikisha wakina mama 1,300 waliokuwa na Saratani ya Mlango wa kizazi kuanza kupatiwa matibabu katika Taasisi ya Ocean Road iliyopo Jijini Dar Es Salaam na kati ya hao 98 wamesha pona na kuruhusiwa kurejea majumbani mwao.

Kauli hiyo ilitolewa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa leo katika mbio za NBC Dodoma Marathon 2023 katika Uwanja wa Jamhuri Mkoani Dodoma.



Mhe. Majaliwa alieleza kuwa katika kipindi cha miaka mitatu iliyopira kupitia mbio za NBC Marathon Dodoma zimefanikisha kukusanya zaidi ya shilingi Milioni 500 na tayari zimesaidia wakina mama 23,000 kupata vipimo mbalimbali vya Afya ya Uzazi

Mhe. Majaliwa alisema Serikali chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassani inaendelea kutekeleza mipango mbalimbali ya kuhakikisha kunakuwa na ustawi wa afya ya mama na mtoto ikiwemo mpango wa Mama Samia Mentorship Program.

Mhe. Majaliwa alisema kuwa mpango mwingine wa Serikali ni kuongeza wigo wa kutoa huduma za kupima dalili za awali za saratani ya uzazi kutoka Vituo vya Afya 925 vilivyopo hadi kufikia vituo vya Afya 1,025

Mhe. Majaliwa alisema katika mbio za NBC Marathon mwaka 2023 inakadiria kukusanya zaidi ya shilingi Milioni 300 ambapo zinatarajiwa pia kutumika katika kuboresha Afya ya Mama na Mtoto.

Kwa upande wake Mwakilishi wa Waziri wa Afya, Mhe .Ummy Mwalimu , ambaye pia ni Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Tumaini Nagu amesemakatika kipindi cha miaka mitatu iliyopita

kuanzia mwaka 2021 mpaka sasa takribani wanawake 40,000 walifikiwa na huduma ya mkoba ambazo zinajumuisha huduma za elimu, uchunguzi wa awali, rufaa na matibabu ya saratani kupitia programu maalumu inayojulikana kama 'Samia Suluhu Hassan Outreach Program'

Aidha Prof. Nagu alitoa rai kwa watanzania kuzingatia mtindo Bora wa Maisha ili kujikinga na Magonjwa Yasiyoambukiza ikiwemo magonjwa ya saratani na kuwaasa wanawake kupima saratani ya mlango wa kizazi kwani endapo itagundulika mapema, Saratani ya Mlango wa Kizazi inatibika na kupona.

# Canada yatoa Shilingi Bilioni140 kwenye Sekta ya Afya

**Na. Majid Abdulkarim, Dodoma**

Serikali ya Canada imetoa kiasi cha Shilingi Bilioni 140 kwenye Mfuko wa Afya ya pamoja (Health Basket Fund) ili kusaidia Sekta ya Afya nchini.

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu alibainisha hayo leo Julai 20, wakati wa mkutano wa utekelezaji wa shughuli za Mfuko wa Afya wa Pamoja (Health Busket Fund) HBF na Waziri wa Maendeleo ya jamii Kanada Jijini Dodoma.

"Tunaishuku sana Serikali ya Canada kupitia Waziri wa Maendeleo ya Kimataifa wa Canada Mhe. Harjit Sajjan kwa kusaidia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kiasi cha shilingi Bilioni 240 kwa ajili ya kuboresha sekta ya afya", alishukuru Waziri Ummy

Aidha, Waziri Ummy alieleza kuwa kati ya kiasi hicho shilingi Bilioni 140 zinaingia serikalini kwa ajili ya kuchangia mfuko wa afya wa pamoja ambapo mpaka sasa Serikali ishapokea kiasi cha shilingi Bilioni 94 ambazo zimeelekezwa kwenye akaunti za ngazi ya msingi ambazo ni zahanati na vituo vya afya nchini.

Alisema, Vituo vya afya na Zahanati watapanga vipaumbele vyao ikiwemo kununua - dawa, uzazi salama, kulipia umeme, kulipia maji na wanatumia kufanya ukarabati mdogo pamoja na kununua vifaa tiba.

"Kwa ujumla mchango wa Serikali ya Kanada kwa Tanzania umeleta matokeo mazuri kwa Huduma za afya Tanzania leo tunaongea wanawake karibu asilimia 90 wajawazito wanajifungulia katika vituo vya kutoa Huduma za afya kwa sababu ya mchango wa Kanada", alisema Waziri Ummy.

Pia aliongeza kuwa wamepunguza vifo vya watoto wachanga na wenye umri chini ya miaka mitano kutoka vifo 67 katika kila vizazi hai 1000 hadi vifo 43.

"Lakini pia tumeweza kupunguza mimba za utotoni kutoka asilimia 27 hadi asilimia 22, tumepunguza udumavu kutoka asilimia 38 na sasa tunazungumzia asilimia 31 na kwa watoto wetu wanapata chanjo", Alisema Waziri Ummy.

Kwa upande wake Waziri wa Maendeleo ya Kimataifa wa Kanada Mhe. Harjit Sajjan alisema kuwa wametangaza miradi mitano mipya ya Afya yenye thamani ya dola za Kanada Milioni 128.5 ambapo dola za Kanada Milioni 75 kwa mfukto wa ruzuku wa shughuli za Mfuko wa Afya wa Pamoja (Health Sector Busket Fund, HSBF) kwa Serikali ya Tanzania na nyongeza ya dola za Kanada 50



# Serikali kupunguza Uagizaji wa Bidhaa za Afya Kutoka 80% hadi 50% Ifikapo 2030.



**Na. Said Nyaoza**
**Dar es Salaama**

Kufuatia jitihada za Serikali katika uwekezaji kwenye eneo la bidhaa za dawa katika Sekta ya Afya Wizara imedhamiria kupunguza uagizaji wa bidhaa za Afya ikiwemo dawa kutoka zaidi ya asilimia 80 hadi chini ya asilimia 50 ifikapo mwaka 2030.

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu alisema hayo leo Julai 21, 2023 kwenye hafla fupi iliyofanyika Hotel ya Johari Rotana na kuwakutanisha wadau pamoja na wawekezaji mbalimbali ambao ni wasambazaji wa bidhaa za Afya.

“Katika mazungumzo yenu tunatumai mtaunga mkono juhudi za Serikali za kuhakikisha tunapunguza uagizaji wa bidhaa za Afya kutoka zaidi ya 80% hadi chini ya 50% ifikapo 2030”, alisema Waziri Ummy

Aidha, Waziri Ummy alisema Serikali kupitia Wizara ya Afya imedhamiria kuvutia uwekezaji katika Sekta ya Afya ikiwemo kuanzisha viwanda vya kuzalisha bidhaa za Afya nchini Tanzania ikiwemo Dawa.

“Tunaendelea kuimarisha viwanda vyetu lakini pia Soko tunalo na tunaungana na nchi nyingine nyingi kupitia kanda za EAC na SADC ili upatikanaji wa huduma bora za Afya uwe rahisi na tuendelee kupata wawekezaji”, alisema Waziri Ummy

“Serikali kupitia Wizara ya Afya tunawakikishia wadau na wawekezaji wetu tutaendelea kusaidia katika uwekezaji wa huduma za Afya ikiwa ni pamoja na soko - la bidhaa zitakazozalishwa”, alisema Waziri Ummy

Alisema, Serikali chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan inaendelea kuimarisha na kuboresha mfumo wake wa Afya kupitia ahadi yake ya kugharamia huduma za Afya ambapo katika mwaka wa fedha 2023/2024 imetengewa zaidi ya shilingi bilioni 600

Mwisho, Waziri Ummy aliwataka wawekezaji hao kuendeleza mazungumzo katika mkutano huo wa "Chat and Dine" ili kuleta matokea mazuri ya wauzaji bidhaa, mawakala, wafanyabiashara wa bidhaa za Afya na wazalishaji wa ndani ili Serikali iendelee kuboresha huduma hizo.



# Serikali kushirikiana na TAMWA katika masuala ya Afya ya Uzazi Mama na Mtoto

**Na Hassan Kimweri,**
**Dar Es Salaam**

Serikali kupitia Wizara ya Afya imedhamiria kushirikiana na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) katika kupambana na kutoa elimu juu ya masuala ya Afya ya Uzazi Mama na Mtoto.

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu aliyasema hayo leo Julai 22, 2023 wakati akizindua rasmi Utafiti wa Haki ya Afya ya Uzazi kwa Wanawake wa Mjini na Vijijini Kupitia Vyombo vya Habari Jijini Dar es Salaam.

“Tunataka tushirikiane kwa pamoja kati ya Serikali na TAMWA juu ya masuala haya ya Afya ya Uzazi Mama na Mtoto kwa kutoa elimu sahihi kwa wananchi ili waweze kujikinga na mimba zisizotarajiwa na magonjwa ya zinaa”, alisema Waziri Ummy

Aidha, Waziri Ummy alisema tafiti hiyo imesaidia kupata Takwimu sahihi ambapo asilimia 81 ya Wanawake wajawazito wanajifungua katika vituo vya kutolea huduma za Afya kwa kuwa wanaimani na vituo hivyo.

Alisema, matokea ya wanawake kujifungua kwenye vituo vya kutolea huduma za Afya ni pamoja na kupungua kwa vifo vya watoto chini ya miaka Mitano kutoka vifo 67 katika kila vizazi hai 1,000 hadi vifo 43.

“Lakini pia, vifo vya watoto chini ya umri wa mwaka Mmoja vimepungua kutoka vifo 43 katika kila vizazi hai 1,000 hadi vifo 33”, alisema Waziri Ummy

Waziri Ummy alisema Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan inaendelea kuboresha huduma za Afya ya uzazi na kuwalinda wasichana, wanawake na watoto kutokana na unyanyasaji wa kijinsia na unyanyasaji dhidi ya watoto.

“Katika juhudi hizi tunazofanya pia, tumefanikiwa katika Afya ya Uzazi kwa kupunguza kiwango cha mimba za utotoni kutoka asilimia 27 ya mwaka 2015/16 hadi asilimia 22 kwa mwaka 2022”. Alisema Waziri Ummy.

Aidha, Waziri Ummy aliwataka wataalam wa Afya ya Uzazi mama na Mtoto kuvitumia vizuri vyombo vya habari kwa kutoa elimu kuhusu Afya ya uzazi kwa watoto wetu lakini tuzingatie mila zetu, desturi na taratibu za Kitanzania.





# Pungiuzeni Semina, Wananchi wapate huduma Vituoni



**Na. Hassan Kimweri, Simiyu**

Waziri wa Afya, Mhe. Ummy Mwalimu amewataka wataalamu wa afya nchini kupunguza semina ili kuwa na muda zaidi wa kutoa huduma bora za matibabu kwa wananchi.

Waziri Ummy alisema hayo leo Julai 10, 2023 katika ziara yake Mkoani Simiyu wakati akizungumza na viongozi wa Mkoa huo chini ya Mkuu wa Mkoa Dkt. Yahaya Nawanda.

“Wataalamu wa afya punguzeni semina maana mmekuwa na semina nyingi hadi kupelekea wagonjwa kukosa huduma kwa wakati na kumekuwa na msomgamano mkubwa katika vituo vya kutolea huduma za afya sababu ya semina”, alisema Waziri Ummy

Aidha, Waziri Ummy alisema kuwa katika utolewaji wa huduma za afya nchini hakuna kilichosimama kwakuwa Serikali imejenga majengo ya hospitali, imetoa dawa na vifaa tiba, hivyo ni jukumu la wataalamu wa Afya kutoa huduma bora patika vituo hivyo.

“Tunamshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutupatia kila kitu katika Sekta ya Afya ikiwemo majengo, vifaa tiba, kuajiri wataalamu na sasa ni jukumu letu wataalamu kutoa huduma bora kwa wananchi kwani ndio dhamira ya Serikali”, alisema Waziri Ummy.

Pia, Waziri Ummy aliutaka uongozi wa Mkoa wa Simiyu kuwasimamia madaktari ili wafanye kazi kwa weledi kwa kuangalia historia ya mgonjwa ili apate huduma sahihi na kwa wakati.

Aliongeza kuwa, lengo la Serikali ni kutoa huduma bora za Afya kwa Watanzania na kwa mara ya kwanza Serikali imetoa hela za dawa kwa asilimia 100, hivyo amevitaka vituo vyote vya Afya kuwa na Dawa zote muhimu ili kumsaidia mwananchi kupata huduma za matibabu kwa wakati.

Hata hivyo, Waziri Ummy alitoa rai kwa watoa huduma nchini kuzingatia utumiaji wa lugha nzuri, weledi na maadili na kuzingatia viapo vya wataalam wa afya wakati wa kuwahudumia wananchi.





# Watu 86 Mkoani Tanga kufanyiwa Upasuaji wa Kurekebisha Viungo

**Na. Catherine Sungura, Tanga**

Jumla ya watu 86 Mkoani Tanga wanatarajiwa kufanyiwa upasuaji wa kurekebisha viungo na kati yao 43 washafanyiwa chini ya Kambi maalum ya Upasuaji wa Viungo (Reconstructive & Cosmetic Surgery) inayoendelea katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Tanga (Bombo).

Hayo yalibainishwa na Waziri wa Afya, Mhe. Ummy Mwalimu mara baada ya kutembelea Kambi maalum ya upasuaji wa kurebisha viungo (Reconstructive & Cosmetic Surgery) inayoendelea katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Tanga (Bombo) mkoani humo.

Waziri Ummy Mwalimu alieleza kuwa upasuaji huo unaofanywa na madaktari bingwa kutoka Ujerumani na Tanzania sio kama ule wa 'wadada' wa kisasa bali ni upasuaji wa Viungo ili kuvirejesha katika utendaji wake wa kawaida

Waziri Ummy Mwalimu alishuhudia wagonjwa ambao wamekatwa miguu yote miwili (baada ya kupata ajali au maambukizi yaliyopelekea kukatwa miguu) sasa wanatembea kwa miguu bila fimbo au msaada wowote baada ya kuwekewa 'miguu', ambapo amesema ma hakika ni jambo la kutia faraja na kuendelezwa.

“Kipekee, ninamshukuru sana Professor Juergen Dolderer na Taasisi yake ya Interplast German na University Medical Centre, Bayreuth German kwa kuichagua Hospitali yetu ya Bombo kuwa mshirika wa kutoa huduma hizi hapa nchini ikiwemo kuwajengea uwezo wataalam wetu wa kitanzania kufanya upasuaji wa kurekebisha viungo”, alimshukuru Waziri Ummy

Waziri Ummy alisema mahusiano ya Tanga na Ujerumani ni ya kihistoria na inasadikika kuwa Bombo ndio Hospitali ya kwanza kujengwa na Wajerumani katika ukanda huu wa Afrika Mashariki.

Aliwashukuru Interplast kwa kukubali ombi lake la kuifanya Bombo Hospitali kuwa Kituo cha Umahiri cha Upasuaji wa Viungo (Centre of Excellence on Reconstructive and Cosmetic Surgery) ukanda wa Afrika Mashariki hivyo wanakamilisha taratibu zote zinazohitajika ili kuyapa nguvu maono haya.

Waziri Ummy alisema kuwa Kambi maalum ya upasuaji wa kurekebisha viungo (Reconstructive & Cosmetic Surgery) inayoendelea katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Tanga (Bombo) ilianza Tarehe 17 Julai 2023 hadi leo na Kambi itafungwa tar 28 Julai mwaka huu

# Wizara ya Afya yakabidhi Zimamoto Magari ya Uokoaji yenye Thamani ya Bilioni 1.6

**Na. Catherine Sungura, Dar es salaam**

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu leo Julai 8, 2023 amemkabidhi Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mhe. Inj. Hamad Masauni Magari matatu ya uokoaji yenye zana za kisasa yenye thamani ya shilingi Bilioni 1.6 kwa ajili ya jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwenye hafla fupi iliyofanyika viwanja vya Zimamoto mkoa wa Ilala jijini Dar es salaam.

Waziri Ummy alisema magari hayo yamekuja wakati muafaka ambapo kwa sasa dunia inajiandaa kukabiliana na majanga, dharura na magonjwa ya milipuko hivyo magari hayo yataenda kutoa huduma za awali pindi ajali inapotokea ili kupunguza madhara yatokanayo na ajali au vifo.

Alisema Wizara yake ilianzisha mfumo rasmi wa huduma za dharura nje ya hospitali ikiwemo uokoaji wakati wa ajali ili kuwezesha majeruhi wa ajali kupata huduma ya kwanza eneo la tukio kabla ya kusafirishwa kwenye vituo vya kutolea huduma za tiba

“Huwa naumia sana ajali inapotokea unaona mtu mzima au mtoto anateketea kwa kukosa vifaa vya uokoaji , kwahiyo mfumo huu wa huduma za dharura nje ya hospitali (EMS) ni hatua muhimu utakaoweza kupunguza athari kwa majeruhi ikiwemo ulemavu pia gharama za matibabu kwa Serikali, mwananchi pamoja na vifo”.

“Magari haya yana uwezo wa kunyanyua na kukata vyuma (Rescue Vans) ambayo pamoja na kazi nyingine yataweza kuopoa majeruhi walionasa katika magari yatakayopata ajali na kazi hii itafanywa vyema na wenzetu wa Jeshi la Zimamoto na uokoaji”, alieleza Waziri Ummy

Hata hivyo Waziri Ummy aliongeza mradi huo umekuja kipindi ambacho kumekuwepo na ongezeko la ajali za barabarani nchini na duniani kote hususan nchi zinazoendelea, “Takwimu zinaonyesha kwamba duniani kote inakadiriwa kuwa hutokea ajali za barabarani zipatazo milioni 1.3 kila mwaka”.







Kwa upande wa takwimu kwa hapa nchini Waziri Ummy alisema kumekuwa na ongezeko kubwa la majeruhi wa barabarani ambapo 47% ni majeruhi watokanao na ajali za pikipiki na jumla ya majeruhi wa ajali walioingia kwa dharura katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) na Taasisi ya Tiba ya Mifupa (MOI) kwa mwaka 2021 walipokea majeruhi wa ajali 9,270 na mwaka 2022 walipokea majeruhi wa ajali barabarani 9,933.

“Waziri tutaleta taarifa ili kuweka mikakati ya kudhibiti ajali za barabarani ikiwemo ajali za pikipiki kwa kuangalia ubora wa ‘helmet’ zinazoingizwa hapa nchini kwani tumeona haziwasaidia watu wengi na kwa bahati mbaya upasuaji wa majeruhi wa ajali watu wengi hawawezi kumudu gharama za matibabu na wengine hawana bima ya afya, na hivi sasa nina vijana wengi ambao ndio nguvu ya Taifa wanahitaji miguu bandia”, alisema.

Pamoja na hayo Waziri Ummy alimshukuru Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mara ya kwanza katika uongozi wake kuweza kujenga majengo ya dharura (EMD) hadi ngazi za wilaya yapatayo majengo 81 na hospitali za mikoa majengo 21 pia wodi za wagonjwa mahututi (ICU) 28 katika hospitali za wilaya na 45 katika hospitali za Mikoa, Kanda na Taifa.
Naye, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mhe. Inj. Hamad Masauni aliishukuru Wizara ya Afya kwa kuwapatia magari hayo ambayo yanaenda kuongeza tija na kuondoa changamoto zilizokuwa zinaikabili jeshi hilo na kuahidi kuyatumia magari hayo ipasavyo.

Alisema magari hayo ni dhamira na mapinduzi makubwa katika jeshi hilo inayofanywa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa - Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuona jeshi hilo linakua na vifaa na zana za kisasa katika uokoaji.

“Ni kweli ajali za barabarini zinaangamiza maisha ya watu wengi hivyo kwa mradi huo utaenda kuwasaidia wananchi kwani tayari askari wameshapatiwa mafunzo na kuwa na weledi katika utoaji wa huduma za uokoaji.



# Program ya mabadiliko ya kiutendaji kwa wataalam kusaidia uboreshaji wa ubora wa huduma za Afya

**Na. Englibert Kayombo, Dodoma.**

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu amesema Serikali kupitia Wizara ya Afya imeendelea kuboresha ubora wa huduma zinazotolewa katika Vituo vya kutolea huduma za afya nchini kwa kuanzisha Programu ya mabadiliko ya kiutendaji kwa wasimamizi na watoa huduma za afya (Leadership4 Health Transfomation Program) katika vituo vya umma vya kutolea huduma za afya.

Waziri Ummy amesema Serikali imeboresha Huduma za afya kuanzia ujenzi wa miundombinu ununuzi wa dawa, vifaa, vifaa tiba, vifaa vya maabara, kuajiri na kusoimesha wataalamu kwa lengo la kuboresha Huduma za afya nchini.

Hivyo uongozi na usimamizi mzuri ndani ya sekta ya afya ndio suluhisho la kufikia lengo la ubora wa Huduma za afya kwa wananchi.

Waziri Ummy amesema hayo kupitia ukurasa wake wa twitter Julai 20, 2023 akiwa anawapongeza Taasisi ya Mifupa Mo Taasisi ya Mifupa (MOI) kwa kuanzisha utaratibu wa kuwapigia simu wagonjwa wao ili kupata maoni, ushauri, pamoja na kuwajulia hali kuwa ni jambo la mfano na linafaa kuigwa na taasisi zote za kutolea huduma za afya.

“Hongereni Taasisi ya Mifupa (MOI) pasi na shaka MOI chini ya Uongozi wa Prof. Abel Makubi inakwenda kuwa nzuri zaidi, serikali kwa upande wetu imefanya mengi kuboresha Huduma za afya na sasa tunajikita katika kuboresha ubora wa Huduma za afya nchini”, ameeleza Waziri Ummy

Mnamo Tarehe 12, Mwezi Mei, mwaka huu, Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu akiwa anawasilisha hoja kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la kuridhia na kupitisha Bajeti ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2023/24 mnamo tarehe 12 Mwezi Mei 2023, Mhe.Ummy aliliomba Bunge kupitisha bajeti ya shilingi 1,235,316,516,000 ili Wizara ya Afya iweze kutekeleza kikamilifu vipaumbele 14 vya kuimarisha ubora wa huduma za afya nchini.

Miongoni mwa Vipaumbele hivyo ilikuwa ni ‘Kuboresha ubora wa huduma zinazotolewa katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini kwa kuanzisha programu ya mabadiliko ya kiutendaji kwa wasimamizi na watoa huduma za afya’ (Leadership4Health Transfomation Program)



Alieleza kuwa Serikali imeboresha miundombinu, kuajiri wataalamu na kununua vifaa tiba na dawa sasa ni wajibu wa watoa huduma za afya nchini kufanya kazi kwa uzalendo, weledi na ufanisi wa hali ya juu ili kuweza kutoa huduma bora za afya kwa wananchi.

“Programu hii italenga kuleta mabadiliko ya utendaji kazi wa watumishi wa afya katika vituo vya kutolea huduma afya kwa kuwapima ufanisi wao katika utendaji kazi”, alifafanua Waziri Ummy.

“Tutaanzisha utaratibu wa kupima utendaji wa timu za uendeshaji wa huduma za afya katika ngazi za Vituo, Hospitali, Halmashauri (CHMT) na Mikoa (RHMT) katika maeneo ya maoteo ya dawa, upatikanaji wa dawa, huduma za uchunguzi (maabara na Radiolojia) udhibiti wa kuchina na kuchotora wa dawa, taratibu za kushughulikia malalamiko ya wagonjwa, muda wa kuwahudumia wagonjwa” alisisitiza Waziri Ummy.

“Tuhakikisha utoaji wa huduma za afya unazingatia weledi, maadili na miiko kupitia mabaraza ya kitaaluma na bodi za usajili ikiwemo kuanzisha mfumo wa kuwatambua na kuwapa tuzo wataalam wanaofanya vizuri” alisema Waziri Ummy.




# India kushirikiana na Tanzania katika upatikanaji wa Dawa za bei nafuu.

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu ametoa wito kwa uongozi wa Hospitali za BLK-Max na MAX-Saket kuendelea kushirikiana na Tanzania katika utoaji wa huduma za matibabu ya kibingwa bobezi nchini Tanzania.

Waziri Ummy alitoa wito huo Julai 26, 2023 wakati akiendelea na ziara yake nchini India, ambapo ametembelea Hospitali za BLK - MAX Speciality Hospitali na MAX-Saket zilizopo mjini New Delhi na kueleza nia ya kuendeleza ushirikiano kwenye matibabu ya ubingwa bobezi kwenye magonjwa ya moyo na mishipa ya damu, ini, figo, saratani, ubongo na mishipa ya fahamu.

"Naishukuru Hospitali za BLK-MAX Speciality na MAX-Saket kwa kuwajengea uwezo wataalam kutoka Tanzania taaluma ya kuanzisha huduma za kupandikiza figo katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili mwaka 2017, huduma huduma za upasuaji mkubwa wa moyo katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) na pia . kutoa mafunzo kazini kwa wataalam wa Mifupa na mishipa ya fahamu katika Taasisi ya Mifupa MOI" alisema Waziri Ummy

Hata hivyo, alitumia fursa ya ziara hiyo kuwajulia hali wagonjwa mbalimbali kutoka Tanzania wanaopata huduma za matibabu katika Hospitali ya BLK - MAX ya mjini New Delhi, India.

Waziri Ummy aliwaalika Uongozi wa BLK-Max na MAX-Saket kufungua Matawi ya Hospitali zao nchini Tanzania ili warahisishe utoaji wa huduma kwa wagonjwa wengi zaidi kwani uwekezaji huo utawapunguzia gharama za safari na muda kwa Watanzania na wananchi wengi wa Afrika Mashariki.

Hospitali hizo kubwa za kisasa zinatoa huduma mbalimbali za kawaida na za ubingwa bobezi ambapo wana madaktari bingwa na bobezi zaidi ya 4800 katika fani mbalimbali na zinauwezo wa kuhudumia wagonjwa zaidi ya milioni 3.5 kwa mwaka kutoka katika nchi zaidi ya 135.



# Waziri Ummy aagiza usajili Zahanati 10 zilizojengwa kwa nguvu ya Wananchi Itilima.

**Na Hassan Kimweri**
**Itilima, Simiyu**

Waziri wa Afya Mhe.Ummy Mwalimu ameagiza kukaguliwa na kusajiliwa kwa zahanati 10 zilizojengwa kwa ushirikiano wa nguvu za wananchi Wilayani Itilima.

Hatua hiyo inalenga kuhakikisha Wananchi Wilayani Itilima wanapata huduma za afya karibu na mazingira wanayoishi Ili kutimiza azma ya Serikali katika kutoa huduma bora za Afya.



Waziri Ummy alitoa agizo hilo Tarehe 11 Julai 2023 Wilayani Itilima baada ya kupokea Taarifa ya Hali ya utoaji huduma za Afya Wilayani humo ambapo katika Taarifa hiyo Mganga Mkuu wa Halmashauri hiyo Bw. Costantine Emanuel Constantine alieleza uwepo wa Zahanati ambazo zimejengwa Kwa nguvu za Wananchi ambazo bado hazijasajiliwa.

"Tusicheleweshe mambo, ili zahanati isajiliwe lazima iwe na nyumba ya mtumishi tutaangalia namna ya kufanya lakini kwa sasa ni muhimu zahanati hizo kusajiliwa na zianze kufanya kazi mara Moja"alisisitiza Mhe. Ummy.

> "zahanati hizo zianze kufanya kazi mara moja baada ya ukaguzi kukamilika na kusajiliwa."



# "Shirika la Madaktari Afrika" lasaidia JKCI Vifaa Tiba vya Bilioni Moja.

**Na. Rayson Mwaisemba**
**Dar Es Salaam**

Shirika la "Madaktari Afrika" lililopo nchini Marekani limetoa msaada wa vifaa tiba vyenye thamani ya shilingi bilioni moja ambavyo vitatumika katika kambi maalumu ya siku tano ya matibabu ya mfumo wa umeme wa moyo wa watu wasiokua na uwezo.

Kambi hiyo ilianza katika Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) ililenga kuwahudumia wagonjwa wasio kuwa na uwezo ambao wamefanyiwa uchunguzi na kupatiwa matibabu katika taasisi hiyo.

Licha ya kutoa vifaa tiba hivyo madaktari hao pia walibadilishana uzoefu baina ya wataalam wa afya wa JKCI na wenzao kutoka Shirika la Madaktari Afrika.

Alizungumza na madaktari wanaotoa matibabu katika kambi hiyo alipowatembela jijini Dar es Salaam Naibu Waziri wa Afya Mhe. Dkt. Godwin Mollel aliwashukuru Madaktari Afrika kwa msaada walioutoa na kusema magonjwa ya mfumo wa umeme wa moyo ni sehemu ngumu kwenye masuala ya tiba ya moyo hivyo amewapongeza madaktari hao kwa kuwa mstari wa mbele kushirikiana na wataalam wa JKCI kuokoa maisha ya watanzania.

“Rais wetu alishawekeza mtambo wa kisasa wa kutibu umeme wa moyo, -upande wa suala la tiba tumejitahidi kupata wataalam wenye uwezo wa kutoa huduma bora kuendana na teknolojia iliyopo, hatuna budi kushirikiana nanyi kwani muda mrefu mmekuwa mkitoa matibabu haya”, alisema Dkt. Mollel.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) Dkt. Peter Kisenge alisema madaktari kutoka Shirika la Madaktari Afrika wamekuja na vifaa tiba vyenye thamani ya shilingi bilioni moja ili kuwasaidia wagonjwa wasiokuwa na uwezo wa kugharamia matibabu hayo.

“Madaktari Afrika ni marafiki zetu ambao wamekuwa wakishirikiana nasi kwa muda mrefu, wamefika hapa kwaajili ya kuwajengea uwezo madaktari wetu na kuwasaidia wagonjwa wenye matatizo ya mfumo wa umeme wa moyo kutokufanya kazi vizuri”, alisema Dkt. Kisenge.

Dkt. Kisenge alisema katika kambi hiyo wagonjwa wenye matatizo makubwa ya mfumo wa umeme wa moyo watapatiwa matibabu na mabingwa hao wakiwa na lengo la kutoa huduma za matibabu pamoja na kubadilishana uzoefu na madaktari, wauguzi na wataalam wa kuendesha mtambo wa Cathlab.

# Dkt. Mollel aahidi Mashine ya CT SCAN Hospitali ya Ligula - Mtwara



**Na. Rayson Mwaisemba, Mtwara**

Naibu waziri wa Afya Dkt. Godwin mollel amekutana na kufanya Kikao na Watumishi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mtwara Ligula na kusikiliza Maoni na Changamoto Mbali Mbali zinazo wakabili katika Sekta ya Afya.

Akizungumza katika kikao icho Naibu waziri alisisitiza kutatua Changamoto mbali mbali zinazowakabiri Watumishia hao na Hospitali



kwa ujumla ikiwemo kilio cha muda Mrefu cha Hospitali hiyo juu ya Upatikanaji wa Mashine uchunguzi wa tishu na ogani za mwili kwa kutumia Mionzi(CT Scan)

Aidha Dkt.Mollel aliahidi kufanyiwa kazi kwa Haraka Ombi la Hospitali hiyo la Kupata mashine ya CT scan.
Dkt Mollel aliwapongeza na kuwashukuru watumishi hao kwa kujumuika nae katika kikao icho kilichofanyika Baada ya Ziara ya uwekaji wa jiwe la Msingi katika Jengo jipya la Wagonjwa wa nje (OPD) lililowekwa na Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa



# Kigoma kupata Ambulance 17 kwaajili ya kubebea Wagonjwa

**Na. Emmanuel Malegi**
**KIGOMA**

Naibu Waziri wa Afya Dkt. Godwin Mollel amesema kuwa, Mkoa wa Kigoma utapata magari ya kubebea wagonjwa 17 (Ambulance) zitazosaidia kutatua changamoto ya huduma za Rufaa na pamoja na vifo vya mama na mtoto katika Mkoa huo.

Dkt. Mollel alisema hayo alipofanya ziara ya kukagua hali ya utoaji huduma na maendeleo ya ujenzi wa miundombinu pamoja na upatikanaji wa vifaa tiba katika hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kigoma.

Alisema, Serikali imenunua jumla ya magari ya kubebea wagonjwa 727 ambayo inatarajia kugawa nchi nzima, huku akibainisha kila Halmashauri inatarajia kupata magari mawili na hospitali ya Mkoa kipata gari moja hali itayosaidia kupunguza changamoto ya uhaba wa magari hayo katika Mkoa.

"Tumenunua Ambulance 727, na tayari Ambulance hizo zimeanza kuingia, - na Tumekubaliana angalau zifike Ambulance 200, kuna uwezekano wa kila Halmashauri kupata Ambulance mbili na kila hospitali ya Mkoa kupata Ambulance, hivyo kuna uwezekano wa mkoa wako kupata Ambulance 17 zitazosaidia kupiga hatua katika huduma za Afya", alisema.

Aidha, Dkt. Mollel aliwapongeza Watoa huduma wa hospitali ya Rufaa ya Mkoa Maweni kwa jitihada na ubunifu wanaoendelea kuonesha katika kuboresha huduma kwa wananchi, hali iliyopelekea kupunguza Rufaa za wagonjwa ndani ya Mkoa huo kwa zaidi ya asilimia 28 ndani ya muda mfupi, huku malengo yakiwa kupunguza asilimia zaidi ya 90.

Katika kuhakikisha upatikanaji wa bidhaa za dawa katika hospitali hiyo Dkt. Mollel aliwataka viongozi wa hospitali hiyo kuhakikisha wanakuwa na Washitiri wazuri na wenye lengo la kuwasaidia

wananchi kwa kufuata vigezo na taratibu zote ili kuhakikisha hakuna changamoto ya - upungufu wa dawa katika vituo vyote vya kutolea huduma", amesema,

Nae, Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kigoma (Maweni) Dkt. Binaga alisema Hospitali itaendelea kushirikiana na Serikali kuu kutenga fedha kwaajili ya maendeleo ya miradi mbalimbali inayoendelea katika hospitali hiyo ili kuhakikisha inamalizika kwa wakati na wananchi wanaanza kunufaika na huduma katika miradi hiyo.

Sambamba na hilo aliongeza, Hospitali inaendelea kutoa huduma kwa njia ya mikoba (outreach) inayowafuata wagonjwa katika jamii na kuwahudumia katika mazingira yao hali iliyosaidia kuboresha afya za wananchi.

Pia, alisema kutokana na kutoa huduma bora kwa wananchi, Hospitali imeendelea kupokea wagonjwa mbalimbali kutoka nje ya nchi ikiwemo nchi ya Burundi wanaofika kupata huduma kupitia hospitali hiyo ya Maweni.





# Watoa huduma za Afya Nchini watakiwa kutoa huduma bora kwa matarajio ya Wananchi

**Na. Emmanuel Malegi**
**Dar es Salaama**

Serkali kupitia Wizara ya Afya, imewataka watoa huduma za afya nchini kuanzia ngazi ya jamii mpaka Hospitali ya Taifa kuweka mikakati ya kutoa huduma bora na zinazokidhi matarajio ya wananchi kwa wakati kwa kutumia lugha yenye staha na unyenyekevu kitu kitakachowafanya waone matunda ya uwekezaji wa Serikali yao.

Wito huo ulitolewa Jijini Dar Es Salaam na Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Dkt. Seif Shekalaghe wakati alipokutana na Wakurugenzi Watendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete na Taasisi ya Tiba ya Mifupa Muhimbili-MOI ili kujadiliana namna ya kuendelea kuboresha ubora wa huduma zinazotolewa na hospitali hizo.

Dkt. Shekalaghe alibainisha kuwa Serikali ya Awamu ya Sita imefanya uwekezaji mkubwa ambao umehusisha ujenzi wa Zahanati, Vituo vya

Afya, hospitali za wilaya, Hospitali za Rufaa za Mikoa na Hospitali za Rufaa za Kanda, -kuongeza hali ya upatikanaji wa dawa, ununuzi wa vifaa tiba na kuajiri watalaamu wenye weledi wa kada mbalimbali za afya.

Alisema kuwa Wananchi wanategemea huduma bora wanapofika hospitalini kupata huduma za afya kwani serikali imetekeleza wajibu wake kwa kuboresha miundombinu na kuhakikisha vifaa tiba vinapatikana katika hospitali zote.

“Niwapongeze sana viongozi kwa kuendelea kutoa huduma bora kwa wananchi, Serikali imekuwa ikijivunia huduma zenu, hizi hospitali ndio taswira ya taifa katika utoaji wa huduma hivyo ninyi mkifanya vibaya mnaharibu taswira ya nchi nzima” alisema Dkt. Shekalaghe

Vile vile, aliwataka viongozi hao kuendelea kuzijengea uwezo Hospitali za Rufaa za Mikoa katika mkoa wa Dar es Salaam kwa kuwa zina vifaa tiba, mashine za uchunguzi na wataalamu kitu kitakachosaidia kupunguza msongamano katika hospitali hizi na zenyewe ziweze kujikita katika huduma za kibingwa na ubingwa bobezi.

Aidha, Dkt. Shekalaghe alitoa rai kwa wananchi kufuata ushauri wa wataalamu wa afya pale wanapopewa maelekezo kwa kuwa wataalamu hao wana weledi wa kutosha na ushauri wao huwa unazingatia taratibu za kiafya.

Mwisho, kikao hicho kiliwashirikisha Wakurugenzi wa taasisi hizo, Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Tumaini Nagu, Mkurugenzi wa Huduma za Tiba kutoka Wizara ya Afya Prof. Paschal Rugajo, Kaimu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Tiba na Sayansi Shirikishi Muhimbili Prof. Appolinary Kamuhabwa.



# Wamiliki wa Maduka ya Dawa Nchini fuateni utaratibu sahihi wa utoaji wa Dawa



**Na. Said Nyaoza**
**Tanga**

Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya Dkt Seif Shekalage amewataka wamiliki wa maduka ya dawa nchini fuateni utaratibu sahihi wa utoaji dawa kwa wagonjwa kulingana na maelezo ya cheti cha dakitari.

Dkt. Shekalaghe alitoa agizo hilo leo Jijini Tanga wakati wakufungua kongamano la mrejesho wa Tafiti za Kukinga na kudhibiti Maambukizi na Usugu wa dawa za Antibiotic katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tanga Bombo.

Dkt. Shekalaghe alieleza kuwa jambo hilo ni la msingi na Serikali wameweka sheria kali kwa mtu atakayekatwa atachukuliwa hatua lakini sasa wanazungumza wanaofanya kwa njia za siri ambao hawajagundulika wanasababisha tatizo linakuwa kubwa kwa jamii.

"Katika hili napenda kusisitiza wamiliki wa maduka ya dawa nchini wafuate taratibu zilizowekwa na Serikali wasitoe dawa kwa wagonjwa kama hawajakwenda na cheti cha daktari", alisisitiza Dkt. Shekalaghe

Aidha Dkt. Shekalaghe alitoa wito kwa waandishi wa habari nchini kutumia kalamu zao kuweza kutoa elimu kwa wananchi juu ya uelewa wa athari za dawa bila kufata utaratibu

Vile vile alisema kuwa zipo dawa muhimu zilizowekwa kwenye maduka lakini dawa za antibayotiki wananchi wasitumie tu kufata utaratibu wa kuwa na cheti cha Daktari.

"Kutumia dawa bila cheti cha Daktari au ushauri wa daktari mtu unatengeneza mwili wako kuwa na usugu wa vimelea vya dawa mwilini ambapo ukipata dawa sahihi zitashindwa kufanya kazi", alieleza Dkt. Shekalagh

Awali alizungumza Mkurugenzi Mtendaji wa NIMR, Prof. Said Abood ametoa wito kwa wananchi kutokununua dawa bila bila cheti cha daktari kwani kumekuwa na mazoezi wananchi kwenda kujinunulia dawa bila kujua kama kweli wanahitaji kutumia hizo.

Pia Prof. Abood alisema kuwa wanapoandikiwa dawa za daktari wahakikishe wanatumia dozi kamili na wanatumia kwa mujibu ilivyoandikwa na Daktari husika.

Aidha aliwataka wananchi kuhakikisha kwamba wanafata utaratibu na matumizi sahihi ya dawa kulingana na cheti cha daktari na kuachana na mambo ya kujitibu wenyewe wanapopata tatizo la kiafya waende hospitalini waonwa na madaktari wapimwe wapate vipimo vya maabara





# Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa Kinara katika kuboresha Huduma za Utengamao na Tiba Mazoezi, Matengenezo ya Vifaa Tiba na Miundombinu.

**Na. Majid Abdulkarim, Iringa**

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Afya Dkt. Grace Magembe amezitaka Hospiatali za Rufaa nchini kuhakikisha zinatoa huduma za utengamao na tiba mazoezi ili kuwezesha wananchi wenye uhitaji wakiwemo watoto wenye ulemavu kuishi maisha yenye ubora na kuweza kujihudumia wao wenyewe

Dkt. Magembe alitoa wito huo leo Mkoani Iringa katika ziara ya kikazi inayofanywa kwa pamoja na Naibu Katibu Mkuu TAMISEMI Dtk.Charles Mahera kukagua utoaji na ubora wa huduma kuanzia ngazi ya msingi hadi rufaa, ambapo wamekagua hali ya utoaji Huduma katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Iringa na Hospitali ya Halmashauri ya Iringa Frelimo.

Viongozi hao walijionea namna Hospitali hiyo ilivyokuwa na karakana ya kisasa ya kutengeneza viungo bandia ikiwemo miguu, mikono na vifaa saidizi mbalimbali.

Waliweza kupata ufafanuzi kutoka kwa wataalamu waliobobea katika taaluma ya -kutoa huduma za utengemao na mazoezi tiba waliopo katika Hospitali hiyo.

Pia, waliona karakana ya kisasa yenye uwezo wa kufanya matengenezo na marekebisho vifaa tiba vyote vya hospitali hiyo pamoja na Hospitali za Wilaya, Vituo vya Afya na Zahanati za Mkoa wa Iringa.

“Niwapongeze kwa kuwa na karakana hii kubwa na nzuri ya kutengeneza vifaa tiba na viungo bandia ambayo ina saidia Mkoa mzima ikiwemo vituo vilivyopo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa”, aliwapongeza.

"Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Dkt Samia Suluhu Hassan imetoa fedha nyingi kununua vifaa tiba vya kisasa kuanzia ngazi ya msingi hadi taifa, ni lazima tuwe na mpango wa matengenezo, ili vikiharibika kidogo visiwekwe stoo kwani itakuwa ni hasara kwa serikali na kuwanyima wananchi huduma”, alisisitiza Dkt. Grace.



# Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya kujikita katika Ubingwa Bobezi na Tiba Utalii



**Na. Majid Abdulkarim, Mbeya**

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Dkt. Grace Magembe ameitaka Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya kujikita katika Ubingwa bobezi na Tiba Utalii na kuwa chanzo za fedha za kigeni katika lango kuu la ukanda wa Nchi za SADC.

Dkt. Magembe alitoa kauli hiyo leo Jijini Mbeya wakati akikagua utoaji wa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi wakati wa ziara yake katika Mkoa Mbeya kufuatia maboresho makubwa yaliyofanywa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Chini ya uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

"Tunakila sababu ya kujikita katika Tiba Utalii kwani tupo imara kuanzia wataalamu bobezi, miundombinu na vifaa tiba vya kisasa ikiwemo MRI, CT scan, vifaa vya upasuaji kutumia tundu dogo, dawa na vitendanishi. Hospitali ya Kanda Mbeya sasa inakuwa kitovu cha ubingwa na ubingwa bobezi kwa nchi zote zinazotuzunguka, andaeni mkakati wa mawasiliano kutangaza huduma hizi" alisisitiza Dkt. Magembe.

"Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Mbeya ni miongoni mwa Hospitali zilipo katika mpango maalum wa kuanzishiwa wa huduma ya matibabu ya mionzi kwa wagonjwa wa saratani. Tunamshukuru Mhe Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuboresha na kusogeza huduma za afya karibu na wananchi kuanzia ngazi ya msingi hadi Taifa"

Aidha, Dkt. Grace alitoa wito kwa Uongozi wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Mbeya na Hospitali ya Mkoa kuweka utaratibu wa kuzijengea uwezo kwenye hospitali za Wilaya, Zahanati na Vituo vya Afya kwa lengo la kuwa-ongezea ujuzi watumishi katika ngazi ya msingi ili kuendana na uwekezaji uliofanywa na serikali.

Dkt. Grace alipongeza maendeleo ya utekelezaji wa mradi wa Ujenzi wa Jengo la Huduma ya Afya ya mama na mtoto katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya pamoja na ujenzi wa vyumba vya upasuaji, wodi na jengo la utakasishaji katika Hospitali ya rufaa ya Mkoa wa Mbeya na kuwataka waongeze kasi na kuhamishia huduma kwenye majengo hayo ifikapo Oktoba 2023





# Serikali kutoa mafunzo kwa wahudumu wa Afya ili kuboresha Huduma

**Na. Shaban Juma**
**Dodoma**

Serikali kwa kushirikiana na shirika la MUSO Health imepanga kuimarisha mifumo ya kutolea huduma za afya ngazi ya jamii.

Hayo yamebainishwa na Mganga Mkuu wa Serikali Prof. Tumaini Nagu mapema leo Julai 27, 2023 ambapo alikutana na ujumbe kutoka shirika la MUSO Health katika kikao cha pamoja kilichofanyika katika ukumbi wa Wizara ya Afya Jijini Dodoma.

Prof. Nagu amesema Serikali ina mkakati wa kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa huduma za Afya kwenye jamii ili kuboresha utolewaji wa huduma za Afya ngazi ya jamii nchini.

"Mafunzo haya yatadumu kwa muda wa miezi sita kwa ajili ya kuwajengea uwezo watoa huduma katika vituo vya Afya ngazi ya Jamii kutoa huduma bora kwa wananchi ili kupunguza kasi ya magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza". Amesema Prof. Nagu.

Aidha, Prof. Nagu amewapongeza Shirika la MUSO Health kwa jitihada wanazofanya katika kuimarisha mifumo ya kutolea huduma za afya katika ngazi ya jamii kwani ni fursa ya kujifunza mifumo mizuri ya uboreshaji huduma za afya ngazi ya jamii.

Kwa upande wake mwakilishi wa MUSO HEALTH, Bi. Laura Musonye amesema ziara yao nchini Tanzania ni kuangalia jinsi huduma za afya zinavyotolewa ili kukabiliana na changamoto za mifumo ya utolewaji wa huduma za afya katika ngazi ya jamii.

Hata hivyo Bi. Laura ameipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuimarisha mifumo ya huduma za afya ikiwemo miundo mbinu, vifaa, vifaa tiba na huduma zinazotolewa katika vituo vya kutolea huduma za afya katika ngazi ya jamii.






# Dkt. Kikwete akoshwa na Huduma za Muhimbili

**Na. Mwandishi Wetu,**
**Dar Es Salaam**

Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete ameipongeza Hospitali ya Taifa Muhimbili Upanga na Mloganzila kwa huduma nzuri wanazotoa kwa jamii na kuwataka wataalamu kuendelea kuchapa kazi kwa bidii na weledi kwakuwa Watanzania wanategemea huduma wanazozitoa.

Dkt. Kikwete alitoa pongezi hizo alipotembela banda la Muhimbili Upanga na Mloganzila katika Maonesho ya 47 ya Kimataifa ya Biashara maarufu saba saba ambapo pia amepata fursa ya kupata huduma katika banda hilo.

“Hongereni sana kwa kazi nzuri na kubwa mnayoendelea kuifanya mkiwa kama Hospitali ya Taifa mnapaswa kuendelea kutoa huduma bora za afya nchini, alipongeza Dkt. Kikwete

Banda la Muhimbili lilikuwa linapatikana katika Ukumbi wa Kilimanjaro ambapo huduma mbalimbali zilitolewa ikiwemo huduma za Magonjwa ya Dharura, Lishe, Macho, ushauri kuhusu afya ya usikivu, vipimo vya msingi vya maabara pamoja na vipimo ya Ultrasound na ECG.



# Chalamila awataka Wananchi kuzingatia ushauri wa Wataalamu wa Afya kuepuka Magonjwa.



**Na. Mwandishi Wetu,**
**Dar Es Salaam**

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mh. Albert Chalamila amewataka wananchi kuzingatia ushauri wa afya unaotolewa na wataalamu ikiwemo kula kadri inavyoshauriwa na wataalamu ili kujiepusha na magonjwa yasiyoambukiza ikiwemo magonjwa ya Figo.

Mh. Chalamila alisema hayo wakati wa kuhitimishwa kwa mbio za Figo Marathoni zilizofanyika leo katika viwanja vya mnazi mmoja kwa lengo kukusanya fedha za kusaidia wahanga wa maradhi ya Figo ambazo zimeratibiwa na MNH kwa kushirikiana na taasisi ya Healthier Kidney Foundation

“Sisi tulio hai ndio tuna nafasi ya kusikiliza ushauri wa kitaalamu na kuufanyia kazi kwa mustakabali wa afya zetu, huwa nikimsikiliza Prof. Janabi anapotoa elimu naona kabisa vitu vingi anavyofundisha vinanigusa kabisa, ni nafasi ya kila mmoja wetu kupanga kubadilika sasa kwa kuwa tumeshasikia tatizo la Figo ni kubwa” alisema Mh. Chalamira

Aidha aliwataka wananchi kuwa na utaratibu wa kukata bima za afya ili ziweze kuwafaa pindi wanapopata maradhi.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili Prof. Mohamed Janabi aliwataka wananchi kuwekeza katika afya kama ambavyo wanawekeza kwa ajili ya kupata mafao ya uzeeni.

Alisema kuwa asilimia 90 hadi 95 ya wagonjwa wanaochuja damu (Dialysis) katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (Upanga & Mloganzila) wamepata maradhi ya Figo kutokana na changamoto ya shinikizo la juu la damu.

“Tafiti zinaonesha kuwa katika wanaume watano basi mmoja ana shinikizo la juu la damu iwe ana jua au hajui, natoa wito kwa wananchi kuwa na utaratibu wa kufanya uchunguzi wa afya kila mwaka na wanapobainika kuwa na changamoto za shinikizo la juu la damu kutumia dawa kama inavyoshauriwa wa wataalamu” alisema Prof. Janabi






# Wizara ya Afya yazindua utafiti wa kitaifa wa viashiria vya Magonjwa Yasiyoambukiza

**Na. Catherine Sungura**
**Dodoma**

Magonjwa Yasiyoambukiza (NCDs) yanachangia takribani 33% ya vifo vyote nchini huku kwa takwimu za Shirika la Afya duniani (WHO) kwa mwaka 2020 zinaonesha kuwa magonjwa hayo yalichangia zaidi ya vifo milioni 41 sawa na 71% ya vifo vyote Duniani ukilinganisha na vifo milioni 57 kwa mwaka 2016 duniani.

Hayo yalielezwa na Waziri wa Afya kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Mhe. Nassor Mazrui wakati wa Uzinduzi wa Utafiti wa Kitaifa wa Viashiria vya Magonjwa Yasiyoambukiza (STEPS SURVEY 2023) uliofanyika kwenye ukumbi wa Takwimu Jijini Dodoma.

Mhe. Mazrui alisema takwimu zinaonesha kuwa magonjwa hayo yameongezeka mara 5 hadi 9 zaidi kati ya miaka ya 80 ambapo 1% tu ya watanzania walikuwa na tatizo la kisukari na 5% walikuwa na tatizo la shinikizo la juu la damu wakati kwa sasa tatizo la kisukari limefikia asilimia 9 na tatizo la shinikizo la juu la damu limeongezeka na kufikia asilimia 25.

"Takwimu hizo zote kutoka katika vituo vyetu vya kutolea huduma za afya nchini - zinaonesha ongezeko kubwa sana la magonjwa hayo ambapo katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Magonjwa Yasiyoambukiza ambayo yalisababisha wagonjwa wengi kuhudhuria vituo vya huduma za afya ni pamoja na shinikizo la juu la damu wagonjwa 1,456,881 sawa na asilimia 49 ukilinganisha na asilimia 34 kipindi kama hicho mwaka 2021/2022 ,Kisukari wagonjwa 713,057 sawa na asilimia 24, magonjwa ya mfumo wa hewa wagonjwa 386,018 sawa na asilimia 13 ikilinganishwa na asilimia 10 kwa kipindi kama hicho mwaka 2021/2022.

Aidha, alisema katika kukabiliana na ongezeko la magonjwa hayo, Serikali inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kupitia Wizara ya Afya imeendelea kutekeleza mkakati wa Kitaifa wa kukabiliana na magonjwa hayo nchini kwa kutoa elimu kwa jamii kuhusu namna bora ya kujikinga na magonjwa hayo pamoja na kuimarisha mifumo ya utoaji huduma za afya nchini kwa kufikisha huduma za uchunguzi wa awali na matibabu kuanzia ngazi ya afya ya msingi.

# Mashine ya MRI imeanza kufanya kazi Hospitali ya Rufaa ya Kanda - Mbeya

**Na Engliber**
**Mbeya.**

Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya leo tarehe Julai 12, 2023 imeanza rasmi kutoa huduma ya vipimo kwa kutumia mashine ya kisasa ya uchunguzi wa magonjwa MRI (Magnetic Resonace Imaging)

Akiongea baada ya kumaliza ziara yake hospitalini hapo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya Mhe. Juma Homera aliishukuru Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uwekezaji mkubwa wa mashine hiyo ambapo ambayo imekua ni hatua muhimu katika kuboresha huduma za afya na kutoa upatikanaji bora wa vipimo vya kisasa kwa wananchi.

"Tunamshukuru sana Mhe. Rais kwa kutoa zaidi ya Shilingi Bilioni 3 kwa ajili ya kufanya uwekezaji huu katika katika Mkoa wa Mbeya ambapo kufanya kazi kwa mashine ya MRI italeta mabadiliko makubwa katika huduma za afya na kuimarisha uwezo wa Hospitali yetu na wataalamu wetu kutoa huduma bora kwa jamii na kupunguza gharama za kusafiri kwenda Dar es salaam kuifuata huduma hii" alishukuru Mhe. Homera

Aidha Mhe. Homera aliishukuru Wizara ya Afya chini ya Mhe. Ummy Mwalimu pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya kwa jitihada kubwa zilizofanyika hadi kufanikisha shughuli za usimikaji wa mashine hiyo ambayo itakuwa na uwezo wa kuhudumia takribani wakazi wa mikoa 7 ya Nyanda za Juu Kusini.

Nae Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya, Dkt. Godlove Mbwanji alisema uwepo wa mashine hiyo utawezesha shuguli za huduma hospitalini hapo kufanyika kwa ubora zaidi kwa kuwa hapo awali wataalamu walikuwa wakilazimika kutoa rufaa kwa wagonjwa kwenda Dar es salaam kufuata kipimo cha MRI.

"Tunaweza kupima wagonjwa ambao wana matatizo ya Saratani au vimbe za aina tofauti tofauti kwenye mwili, pia tunaweza kupima mabadiliko yanayoendana na umri."

Bi. Reinfrida Kayombo mkazi wa Jijini Mbeya, ameishukuru Serikali kwa kwa kuwaletea huduma hiyo karibu na kuwasaidia kwa wakazi wa Nyanda za juu kusini ambao hapo awali walilazimika kutumia garama kubwa kuifuata huduma hiyo mbali.





# Muhimbili imekidhi vigezo kushughulikia dharura za AFCON 2027

**Na Shabani Juma,**
**Dar es Salaam**

Hospitali ya Taifa Muhimbili imefuzu kuwa na uwezo wa kushughulikia dharura za kiafya zinazoweza kujitokeza katika michuano ya Mpira wa Miguu Barani Afrika (AFCON 2027) ikiwa Afrika Mashariki itapewa ridhaa ya kuwa mwenyeji wa michuano hiyo.

Haya yameelezwa na Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Bw. Saidi Yakub ambaye aliambatana na jopo la Wakaguzi kutoka Shirikisho la Mpira wa Miguu Barani Afrika (CAF) ambao wapo nchini kukagua miundombinu muhimu ikiwemo viwanja vya michezo, Hoteli, Viwanja vya ndege na Hospitali.

Katika kukagua leo wamefika hapa hospitali ya Taifa Muhimbili ambapo wamekagua Idara ya Magonjwa ya Dharura na Ajali, mashine za kisasa za uchunguzi lakini pia wamepata maelezo mazuri kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili Prof. Mohamed ambaye ameeleza uwezo na utayari wa MNH katika kutatua dharura zozote zinazoweza kujitokeza" amesema Bw. Yakub

Amesema ukaguzi unakwenda vizuri na kwamba Muhimbili imekidhi vigezo vilivyotakiwa na zinasubiriwa tu baadhi ya nyaraka ambazo wakaguzi hao wameziomba

Awali akiwasilisha mada kwa wakaguzi hao, Mkurugenzi Mtendaji wa MNH Prof. Mohamed Janabi alisema kuwa Muhimbili ndio hospitali kubwa nchini, ikiwa na vitanda 2,150 katika kampasi zake za Upanga na Mloganzila huku ikiwa na wataalamu bingwa wa kada zote, ina mashine za vipimo vya uchunguzi ikiwemo MRI 3, CT Scan 3, Angio Suit 1 pamoja na Idara ya Magonjwa ya Dharura yenye uwezo wa kuhudumia watu wapatao 250 kwa siku.

"Kijiografika katika eneo iliyopo Hospitali yetu kuna Hospitali mbili za Ubingwa wa Juu ambazo ni Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) na Taasisi ya Tiba ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI) ambazo kwa pamoja zina uwezo wa kutatua changamoto yoyote inayoweza kujitokeza" ameeleza Prof. Janabi

Kwa upande wa jopo la wakaguzi wa CAF wakiongozwa na Bw. Lakshmikanthi Karunanithi kwa kiasi kikubwa wameonyeshwa kuridhika na ubora wa huduma na miundombinu iliyopo MNH.

Tanzania imeomba kuwa mwenyeji wa Mashindano ya Mpira wa Miguu barani Afrika (AFCON 2027) kwa kushirikiana na nchi jirani ambazo ni Kenya na Uganda.



# Huduma ya Kiti mwendo yaanzishwa kituo cha Daladala Muhimbili

**Na. Mwandishi Wetu,**
**Dar Es Salaam**

Hospitali ya Taifa Muhimbili imeanzisha huduma ya kubeba wagonjwa wasioweza kutembea kutoka kwenye kituo cha daladala kilichopo nje ya geti la kuingilia hadi katika maeneo ya kutolea huduma kwa kutumia viti mwendo (Wheel chairs)

Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Uuguzi na Ukunga wa MNH, Bi. Redempta Matindi alisema kuwa huduma hiyo ni muhimu kwa kuwa wapo wagonjwa wasiojiweza kabisa kutembea wenyewe.

"Sisi kama watoa huduma tumeona ni vema kuanzisha huduma hii kuwasaidia mwendo wagonjwa ili wafike kwenye maeneo ya kutolea huduma wakishafika huko wanakutana na watoa huduma wa maeneo husika" alisema Bi. Redempta

Alisema huduma hizo zinatolewa na waliokuwa waraibu wa dawa za kulenya ambao wanaendelea na tiba ya Methadone ili kuwasaidia kurejea katika maisha ya kawaida.



# Upasuaji wa Miguu kifundo kufanyika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita.




**Na .Sostheness Mganga, Geita**

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita kupitia Idara ya Tiba ya Viungo na Utengamao imeanzisha huduma ya kliniki ya upasuaji wa Mguu kifundo kwa watoto wadogo wanaozaliwa na changamoto.

Hayo yalibainishwa na Mganga Mfawadhi wa Hospitali hiyo Dkt. Mfaume Kibwana alipokuwa akizungumza na wananchi waliofika hospitalini hapo kupata Huduma mbalimbali katika Idara ya Tiba ya Viungo na Utengamao.

Dkt. Kibwana alieleza kuwa inakadiriwa zaidi ya watoto 2500 hadi 2800 uzaliwa na tatizo hilo kila mwaka nchini.

Dkt. Mfaume alisema kuwa Serikali kupitia Wizara ya Afya, imeendelea kuboresha huduma za afya katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita kwa kuhakikisha Huduma za Ubingwa na bobezi zinapatikana katika hospitali hiyo.

Hivyo kusogeza huduma za Ubingwa na ubingwa bobezi kwa wananchi kutawapunguzia gharama wagonjwa kusafiri nje ya Mkoa wa Geita kufuata huduma hizo.

"Kwa sasa kwenye Hospitali yetu tumezindua rasmi kliniki ya upasuaji wamguu kifundo kwa watoto wachanga ambapo huduma hii itakuwa imepunguza kadhia na gharama kwa wagonjwa kupelekwa nje ya mkoa wa Geita ", alieleza Dkt, Mfaume

Aidha Mganga Mfawidhi Dkt. Mfaume Kibwana aliwataka watumishi wa Idara husika kuhakikisha wagonjwa wanapatiwa huduma iliyobora na uhakika kwani itasaidia kupunguza matatizo ya watoto kuwa na ulemavu katika jamii hasa kama huduma hizo zitatolewa kwa wakati sahihi unaotakiwa na ufanisi.

Dkt. Mfaume aliwasishi watumishi wote wa Hospitali hiyo kuhakikisha wanavilinda na kuvitunza Vifaa na mashine mbalimbali ambazo zinaletwa katikaHospitali hiyo kwa ajili ya kutoa huduma kwa wagonjwa.

"Kwa sasa tunavyo vifaa vyote muhimu kwa hii idara ya Mazoezi na Utengamao wa Viungo naomba mkavitunze, na agizo hili pia liwafikie idara zingine ni lazimatuhakikishe tunatoa huduma bila kukwamishwa na uharibifu wa makusudi wa vifaana vitendea kazi" alisisitiza Dkt. Mfaume.

Kwa upande wake Mkuu wa Idara ya Tiba ya Viungo na Utengamao, Yasinta Mligo alisema kuwa wapo tayari kutoa huduma ya upasuaji kwani mwanzoni walikuwawanatoa huduma za awali bila kufanya upasuaji wa tatizo hilo kutokana uhaba wawataalam na vifaa hivyo kupatikana kwa wataalam na vitendea kazi kutasaidia kuondoa mkwamo wa upatikanaji wa uhakika wa huduma hizo hospitalini hapo.



# Watu 70 hufariki kila siku kwa ugonjwa wa Kifua Kikuu Tanzania

**Na.Hassan Kimweri**
**Arusha**

Watu 70 hufariki kila siku nchini Tanzania kutokana na Ugonjwa wa Kifua Kikuu (TB) na watu 25,800 hufariki kila mwaka kutokana na ugonjwa huo hapa nchini.

Hayo yalielezwa na Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu wakati akifungua Mkutano wa Makatibu Wakuu na Mameneja Mpango wa Programu za Kifua Kikuu kutoka Nchi 15 Barani Afrika unaofanyika kwa Siku Tatu Jijini Arusha.

Waziri Ummy alisema takwimu za kidunia zinaonesha kwamba takriban watu Milioni 10.5 wanaambukizwa ugonjwa wa Kifua Kikuu (TB) kila mwaka na kati yao watu takribani Milioni 1.6 hufariki kutokana na ugonjwa huo.

“Ikitokea basi la abiria limepata ajali na watu 70 wamekufa kila mtu ataandika Rest in Peace lakini Ugonjwa wa Kifua Kikuu unaua watu 70 kila Siku Tanzania ndio maana kwa kushirikiana na Mfuko wa Dunia wa kupambana na Kifua Kikuu, UKIMWI na Malaria (Global Fund) tumeamua kukutana na Makatibu Wakuu wa Wizara za Afya ili tujadili namna ya kuutokomeza ugonjwa huo ifikapo 2030”, alieleza Waziri Ummy.

“Takwimu zinaonesha kwamba takriban watu Mil. 10.5 wanaambukizwa ugonjwa wa Kifua Kikuu (TB) kila Mwaka Duniani na kati ya hao watu takriban Mil. 1.6 hufariki kutokana na ugonjwa huo”, alisema Waziri Ummy

Pia, Waziri Ummy alibainisha kuwa kati ya Watu 100 watu 39 waliibuliwa na ugonjwa wa Kifua Kikuu kwa Mwaka 2015 nchini Tanzania ambapo hadi Sasa Serikali kupitia Wizara ya Afya imepiga hatua kwa kuweza kuibua wagonjwa hao kwa asilimia 65.

"Tumeongeza jitihada za kuendelea kuibua wagonjwa wa Kifua Kikuu kutoka Mwaka 2015 ambapo katika kila wagonjwa 100 tulibua wagonjwa 39 kwa Mwaka huo na kwa sasa tumeweza kuibua wagonjwa kwa asilimia 65 kwa kuwatumia wahudumu wa Afya ngazi ya Jamii", alisema Waziri Ummy

Alisema, Jitihada hizo zimetokana na kuwatumia wahudumu wa Afya ngazi ya Jamii kwa sababu wao ndio wapo karibu na Jamii ambapo wanaweza kupita katika vilabu vya pombe, vijiweni, nyumba kwa nyumba pamoja waganga wa Tiba Asili baada ya kupewa mafunzo ya uelewa wa mgonjwa mwenye Kifua Kikuu.

Lengo la Mkutano huo lilikuwa ni kujadili kwa pamoja ni jinsi gani Nchi za Afrika zinaweza kuja na ubunifu pamoja na mikakati mipya ya kutokomeza Ugonjwa wa Kifua Kikuu Afrika na Duniani kwa ujumla ifikapo Mwaka 2030.






# Wizara ya Afya Kinara wa matumizi ya Kidigitali ya katika utoaji wa Habari

**Na. Englibert Kayombo**
**Dar Es Salaam**

Wizara ya Afya imeendelea kuwa kuwa kinara wa matumizi ya kidigitali ya mitandao ya kijamii katika utoaji wa habari mitandaoni na kwenye vyombo mbalimbali vya habari pamoja na kutumia nyenzo za kidigitali kurahisisha utoaji wa huduma bora za afya kwa wananchi.

Wizara imeibuka mshindi wa Tuzo za Kidigitali kwa Mwaka 2022 katika Kipengele cha Wizara iliyoongoza katika mawasiliano Kidigitali.

Taasisi ya Serengeti Bytes kwa mara nyingine tena wameanda tuzo hizi ambazo hushirikisha Taasisi na Watu wenye ushawishi kwenye jamii waliofanya vyema kwenye matumizi bora ya kidigitali.

Tuzo hizi zimetolewa leo Tarehe 15 Julai, 2023 Jijini Dar Es Salaam na kupokelewa na Mwakilishi sa Katiku Mkuu Dkt. Omary Ubuguyu Mkurugenzi Msaidizi Programu ya Kudhibiti Magonjwa yasiyoambukiza pamoja Bw. Englibert Kayombo Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalino, Wizara ya Afya.

Shukrani ziwaendee Viongozi wetu wakiongozwa na Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu kwa uongozi hodari na kuzingatia umuhimu wa nyezo za kidigitali kuweza kufikisha habari na mawasiliano kwa umma, kutumia nyezo za kidigitali kuweza kurahisisha utoaji wa huduma za afya, Taasisi zote zilizo chini ya Wizara ya Afya, Mabaraza na Hospitali za Rufaa za Mikoa, Waandishi wa habari na wananchi wote kwa kuendelea kufuatilia taarifa mbalimbali za Wizara kwenye mitandao yetu.






# Epuka Magonjwa ya Kuharisha na Kutapika


Hakikisha maji ya kunywa ni safi na salama kwa familia yako




1. Vyanzo vya maji lazima viwekwe safi



2. Chemsha maji ya kunywa



3. Ipua na kuyaacha yapoe



4. Hifadhi maji kwenye chombo safi na kilichofunikwa



5. Tumia chombo kisafi kunywa maji

***Mtu ni Afya; Chukua Tahadhari, Kuharisha na Kutapika Sio Poa***






**Jarida hili limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**
**WIZARA YA AFYA, TANZANIA, TOLEO LA MWEZI JULAI 2023**